**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO NA MWELEKEO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujaalia uhai na uzima na kutuwezesha kukutana tena ili kutekeleza majukumu yetu ya kikatiba ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Aidha, napenda nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii kusimama mbele ya Baraza lako kwa niaba ya Kamati ya Bajeti kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Mwelekeo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa Hotuba hii ni Matakwa ya Kanuni ya 93(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la mwaka 2020) ambayo inaelekeza kwamba, Mapendekezo ya Mwelekeo wa Mpango wa Taifa yatawasilishwa katika Kamati ya Bajeti kabla ya kuwasilishwa Barazani. **Mheshimiwa Spika,** naomba nikuarifu kuwa Kamati yangu imeitekeleza vyema Kanuni hiyo kwa kupokea waraka huo na kufanya majadiliano na Afisi ya Rais Fedha na Mipango. Aidha, katika utekelezaji wa kazi hiyo Kamati yangu pia imezingatia matakwa ya Kanuni ya 93(4) inayoelekeza kuwaalikaa Wenyeviti wa Kamati za kudumu pamoja na Wadau kwa ajili ya kutoa maoni yao kuhusu taarifa hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa naomba niwashukuru Wenyeviti wa Kamati za kudumu za Baraza kwa ushirikiano wao walionipatia kwa kufika mbele ya Kamati ya Bajeti na kutoa maoni yao. Aidha, naomba niwashukuru wadau mbali mbali walioalikwa na Kamati yangu kwa kutenga muda wao na kufika mbele ya Kamati kutoa maoni yao. Sisi Kamati ya Bajeti tunathamini sana michango yao. Napenda kuwahakikishia kuwa maoni na michango yao waliyoiwasilisha ni ya umuhimu mkubwa na imezingatiwa na Kamati yangu wakati wa kufanya majadiliano na Afisi ya Rais Fedha na Mipango na wakati wa kuandaa Hotuba hii.

## MAUDHUI

### MAPITIO YA HALI YA UCHUMI

#### Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar

**Mheshimiwa Spika,** Uchumi wa Zanzibar umeimarika Kwa kipindi cha robo tatu za mwanzo (Januari – Septemba) mwaka 2021 ukilinganisha na kipindi kama hicho cha mwaka 2020. Kuimarika huko kunatokana na kuongezeka kwa idadi ya watalii, kuongezeka kwa miradi ya uwekezaji, kuimarika kwa shughuli za kilimo, kuimarika kwa sekta za kifedha pamoja na kuongezeka kwa mapato ya Serikali Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unakwenda sambamba na mabadiliko ya hali za wananchi kiuchumi pamoja na uboreshaji wa huduma za msingi za jamii kama vile miundombinu ya barabara, huduma za afya, elimu nakadhaalika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Serikali ijikite kuziimarisha kiuchumi sekta zinazogusa wananchi wengi hasa wenye kipato cha chini kama vile sekta ya Uvuvi, Kilimo na Ujasiriamali ili kupunguza umasikini na kuongeza ajira kwa wananchi wa Zanzibar.

#### Ukuaji wa Uchumi

**Mheshimiwa Spika,** Kasi ya ukuaji uchumi wa Zanzibar imekua kama ifuatavyo;

Robo ya kwanza (Jan-Machi) 2021 uchumi umekua kwa kasi ya wastani wa asilimia 2.2 ikilinganiswa na kasi ya asilimia 1.8 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2020.

Robo ya pili (April –June) ya mwaka 2021 uchumi umekua kwa kasi ya wastani wa asilimia 6.5 ikilinganishwa kasi ya asilimia -2.0 kwa kipindi kama hicho cha mwaka 2020.

Robo ya tatu (Julai –Septemba) ya mwaka 2021 uchumi umekua kwa kasi ya wastani wa asilimia 8.8 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 3.3 kwa kipindi kama hicho cha mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuwekeza katika miradi mbali mbali ya kiuchumi, kuimarisha shughuli za kilimo pamoja na kuimarisha sekta ya viwanda kwa lengo la kustawisha kasi ya ukuaji wa uchumi na kuongeza Pato la Taifa.

**Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa**

**Mheshimiwa Spika,** Mchango mkubwa zaidi wa sekta katika Pato la Taifa unachangiwa na sekta ya huduma ambayo imechangia asilimia 46.0 kwa mwaka 2021 kutoka wastani wa asilimia 35.5 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2020. Aidha, Sekta ya pili yenye mchango mkubwa katika Pato la Taifa ni Sekta ya Kilimo ambayo inachangia asilimia 26.3 kwa kipindi cha miezi tisa (Januari-Septemba) cha mwaka 2021 kutoka wastani 29.5 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2021 Sekta ya Viwanda imetoa mchango mdogo katika Pato la Taifa kwa Zanzibar ambayo imechangia asilimia 19.9 kutoka wastani 24.0 kwa mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kutilia mkazo uimarishaji wa Sekta muhimu ambazo zinatoa mchango mkubwa katika kuongeza pato la Taifa kama vile Sekta ya huduma ambayo ndani yake inabeba shughuli za kitalii, biashara, usafirishaji nakadhaalika. Aidha, Sekta ya Viwanda inaonekana kushuka katika uchangiaji wa Pato la Taifa Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuiangalia sekta hii kwa umakini wake na kutatua kwa haraka changamoto zinazoikwaza sekta hii ili iweze kuleta tija kwa wananchi wa Zanzibar na kuweza kutoa mchango mkubwa katika kuongeza Pato la Taifa.

## Mwenendo wa Uingiaji wa Watalii

**Mheshimiwa Spika,** Idadi ya uingiaji  watalii nchini imeongezeka katika kipindi cha miezi tisa (Jan-Sept) kwa mwaka 2021 na kufikia watalii 278,754 sawa na ongezeko la asilimia 80 kutoka watalii 154,848 walioingia katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2020. Kuongezeka kwa idadi ya watalii kunatokana na kupungua kwa kiasi kikubwa athari ya ugonjwa wa UVIKO 19 na kufunguliwa kwa mipaka ya kusafiri kwa baadhi ya mataifa.

**Mhesimiwa Spika,** Ili kubaini ukuaji wa sekta ya utalii ni vyema Serikali ijikite zaidi kutoa takwimu halisi za mapato yanayotakana na uingiaji wa wageni kwani takwimu za idadi ya watalii pekee haitoshi kupima ukuaji wa sekta hiyo. Aidha, suala la kuimarishwa kwa miundombinu ikiwemo barabara za ndani zinazoelekea katika hoteli za kitalii zitasaidia katika kutoa taswira na mandhari nzuri ya maeneo hayo.

## Mwenendo wa Mfumko wa Bei

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonesha kuwa kasi mfumko wa bei za bidhaa imeshuka na kufikia wastani wa asilimia 1.5 kwa kipindi cha miezi tisa (Januari – Septemba) 2021 kutoka wastani wa asilimia 4.2 kwa kipindi kama hicho mwaka 2020, hali hii inatokana na kupungua kwa bei za bidhaa za chakula kama vile sukari, mchele ambazo zimepunguzwa ushuru na Serikali. Kamati inaishauri Serikali kuendelea na mikakati mbalimbali ya kudhibiti kasi mfumko wa bei za bidhaa na huduma ili kuwapa unafuu watumiaji.

## Mwenendo wa Uagiziaji na Usafirishaji wa Biashara Nje ya Nchi

**Mheshimiwa Spika,** Nakisi ya biashara imepungua kufikia thamani ya TZS 586.1 bilioni kwa (Januari – Septemba) mwaka 2021 kutoka thamani ya TZS 601.7 bilioni kwa (Januari – Septemba) mwaka 2020. Kupunguwa kwa nakisi ya biashara kumesababishwa na kuongezeka kwa usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi zenye thamani ya TZS 99.1 bilioni kwa (Januari – Septemba) mwaka 2021 ikilinganishwa na thamani ya TZS 56.8 bilioni kwa (Januari – Septemba) mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Ili uchumi wa nchi ukue unahitaji uzalishaji wa bidhaa za ndani na kuziuza nje ya nchi. Hivyo Kamati inasisitiza kuwekwa mikakakti imara ya kuongeza uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi kwa lengo la kuinua

uchumi wa nchi na kupunguza nakisi ya biashara.

## Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji wa Sarafu

**Mheshimiwa Spika**, Thamani ya Fedha ya Tanzania ilipunguwa kwa kiwango kidogo cha asilimia 0.25 kwa kipindi cha miezi tisa (Januari – Septemba) mwaka 2021 na kufikia wastani wa TZS 2,298.7 kwa dola moja ya kimarekani ikilinganishwa na wastani wa TZS 2,292.8 kwa (Januari – Septemba) mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuendelea kusimamia sera bora za fedha na taasisi husika, kushiriki vizuri katika soko la kuuza na kununua fedha za kigeni ili sarafu yetu ya Tanzania izidi kuwa na thamani zaidi. Vile vile Kamati inasisitiza wananchi katika matumizi yao ya ndani ya kununua bidhaa na huduma kwa kutumia Shilingi ya Tanzania ili kuimarisha thamani ya sarafu yetu.

## MAPITIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2020/2021, kiasi cha makusanyo ya mapato kilifikia TZS 944.6 bilioni sawa na asilimia 59.8 ya makadirio ya kukusanya TZS 1,579.2 bilioni. Aidha, Serikali imefanikiwa kutumia jumla ya TZS 953.8 bilioni. Kati ya fedha hizo, TZS 740.1 bilioni zilitumika kwa kazi za kawaida sawa na 76.4 ya makadirio ya kutumia TZS 969.3 bilioni na kwa upande wa kazi za maendeleo zilitumika TZS 213.7 bilioni sawa na asilimia 35 ya makadirio ya kutumia TZS 609.9 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** Ukiangalia mwenendo wa mapato na matumizi utagundua kwamba tokea awali huwa tunapanga kutumia asilimia ndogo ya mapato kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo. Aidha, katika utekelezaji halisi pia matumizi ya kazi za maendeleo yanatekelezwa kwa asilimia ndogo. Jambo hili linaonesha bado hatujawa na uwezo wa kutosha wa kukusanya mapato na kutekeleza miradi ya maendeleo.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI NA MATARAJIO YA BAJETI KWA MWAKA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha nusu mwaka 2021/2022 (Julai – Disemba 2021/2022), Serikali imefanikiwa kukusanya jumla ya TZS 714.6 bilioni sawa na asilimia 85 ya makadirio ya kukusanya TZS 836.3 bilioni kwa kipindi hicho. Aidha, jumla ya TZS 465.6 bilioni sawa na asilimia 69 ya makisio ya kutumia TZS 672 bilioni zilitumika. Kati ya matumizi hayo, TZS 367.9 bilioni zilitumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 81.7 ya makisio ya TZS 450.2 bilioni na TZS 97.6 bilioni zilitumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 43.8 ya makisio ya TZS 222.6 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na mwenendo wa mapato, matarajio ya Serikali kwa mwaka 2021/2022 hadi kufikia Juni 2022 ni kukusanya jumla ya TZS 1,422.1 bilioni ambayo sawa na asilimia 77.7 ya makadirio ya kukusanya TZS 1,829.9 bilioni. Aidha, matumizi ya Serikali kwa mwaka mzima wa 2021/2022 yanatarajiwa kufikia jumla ya TZS 1,418.7 bilioni. TZS 731.2 bilioni zitatumika kwa matumizi ya kazi za kawaida ikiwa ni sawa na asilimia 77 ya makadirio ya kutumia TZS 947.1 bilioni na kwa upande za maendeleo jumla TZS 690.9 bilioni sawa na asilimia ya 78 ya makadirio ya kutumia TZS 882.8 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi za kukusanya mapato hazifikii malengo ya ukusanyaji, hususani Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB). Takwimu zinaonesha, kwa kipindi cha Julai – Disemba 2021/2022, ZRB imefikia asilimia 65 ya malengo na kwa upande wa TRA imefanikiwa kukusanya asilimia 82 ya malengo yake. Kamati inaishauri Serikali, iweke mkazo mahsusi wa kuiimarisha ZRB hasa katika mifumo yake ya kielektroniki ili iweze kukusanya mapato kwa ufanisi na kuweza kutekeleza hatua za kuwaletea maendeleo wananchi. Hali hii itawapelekea wananchi kujenga imani kwa Serikali na hatimae kutajengeka tabia ya kulipa kodi kwa hiari.

## DENI LA TAIFA

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Disemba 2021, Deni la Taifa limefikia TZS 1,127.5 bilioni ikilinganishwa na TZS 896.6 bilioni Disemba 2020. Hii inamaanisha kwamba, kwa kipindi cha mwaka mmoja Deni la Taifa limeongezeka kwa TZS 230.9 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 25.6. Deni hilo limejumuisha kiasi cha TZS 925.5 bilioni ikiwa deni la nje na TZS 202.2 bilioni ni deni la ndani.

Mheshimiwa Spika, Licha kuwa Deni la Taifa ni himilivu lakini hatuna budi kuweka mikakati thabiti ya kulidhibiti deni hilo. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuongeza vyanzo vipya vya mapato sambamba na kuendelea kuzuia uvujaji wa mapato.

## UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Katika Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2021/2022 kulipangwa kutekelezwa Programu 25 na Miradi 39 na kupangiwa jumla ya TZS 882.8 bilioni. Kati ya fedha hizo, TZS 606.5 bilioni sawa na asilimia 68.7 ni mchango wa Serikali na TZS 276 bilioni sawa na asilimia 31.3 ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha nusu mwaka 2021/2022, jumla ya TZS 97.6 bilioni ikiwa ni asilimia 11.1 ya makadirio ya kutumia TZS 882.8 bilioni kwa mwaka 2021/2022. Kamati inaishauri Serikali kupanga bajeti ambazo zina uhalisia kwani miradi mingi inapangwa kwa miaka kadhaa lakini baadhi ya miradi hiyo hakuna utekelezaji unaofanywa hata wa kazi za awali.

Mheshimiwa Spika, Takwimu zinaonesha upatikanaji wa fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo bado ni mdogo sana na utekelezaji wa baadhi ya miradi bado haijaanza kabisa. Kamati inapata wasi wasi juu ya utekelezaji huo hasa ikizingatiwa kuwa utekelezaji wa miradi ni muhimu katika uchumi na maendeleo ya nchi. Hivyo, Kamati inashauri licha ya kuwepo kwa changamoto ya upatikanaji wa fedha, watendaji waliopewa dhamana ya kusimamia miradi kutekeleza vyema majukumu yao kwa kuhakikisha fedha inayopatikana inatumika kwa mujibu wa malengo na kwa ufanisi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendela kusisitiza kwamba ili utekelezaji wa miradi uwe na ufanisi na hatimae utowe tija, Serikali haina budi kupunguza idadi ya miradi inayopangwa kutekelezwa kwa mwaka ili kuipa nafasi Serikali kutenga kiasi kikubwa zaidi katika kutekeleza miradi michache ambayo itakamilika kwa wakati.

## MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2022

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusiana na takwimu za mwelekeo wa hali ya uchumi kwa mwaka 2022 zinaonesha kuwa, uchumi wa dunia, uchumi wa nchi zinazoendelea, uchumi wa nchi za Afrika Mashariki na Zanzibar zinatarajiwa kuongezeka kwa wastani tofauti kama zinavyooneka katika taarifa ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa takwimu za Zanzibar kwa mwaka 2022 zinatarajiwa kukuwa kwa asilimia 6.5 kutoka asilimia 5.2 mwaka 2021. Kamati inasisitiza kuwa, matarajio haya yaliyopangwa yaende sambamba na kupatikana kwa maendeleo ya uchumi nchini na Serikali kutilia mkazo katika kusimamia sekta ambazo ukuaji wake utawanufaisha wananchi walio wengi.

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu za matarajio ya ukauji wa uchumi pekee itakuwa sio kitu muhimu kwa wananchi wetu, iwapo matokeo yake hayatawasaidia katika kuimarisha maisha yao katika nyanja mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuimarika kwa huduma za afya, upatikanaji wa elimu bora na kupungua kwa umaskini.

## MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2022/2023 umejikita kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa mwaka 2021-2026 (ZADEP), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa mwaka 2020 hadi 2025, Hotuba na ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Maeneo ya vipaumbele yaliyoainishwa katika Mwelekeo ni pamoja na kuimarisha Uchumi wa Buluu, kuimarisha miundombinu, kuimarisha Sekta ya Utalii na kuimarisha huduma za jamii ambapo jumla ya fedha zilizotengwa katika maeneo hayo ni TZS 522.1 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaunga mkono maeneo ya vipaumbele yaliyoainishwa pamoja na kuisisitiza Serikali juu ya kuandaa mipango mizuri ya utekelezaji wa vipaumbele hivyo ikiwa ni pamoja na kuandaa wataalamu nchini katika fani mbali mbali sambamba na kujikita katika masuala ya utafiti katika maeneo hayo ili yaweze kutekelezwa kwa uweledi.

Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha Uchumi wa Buluu ambalo ni eneo jengine la vipaumbele, Kamati inasisitiza Serikali kusimamia kukamilishwa kuandaliwa kwa Mpango wa Matumizi ya Bahari na maeneo yake ili uweze kutumika katika utekelezaji wa shughuli mbali mbali zinazohusiana na uchumi huo. Aidha, wananchi wanahitaji kuelimishwa zaidi juu ya dhana ya Uchumi wa Buluu na umuhimu wake ili nao washiriki ipasavyo na hatimae kuchangia uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha miundombinu, Kamati inaishauri Serikali kupitia eneo hili, kuharakisha utekelezaji wa Miradi ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Barabara, Miradi ya Uimarishaji wa Usafiri wa Anga na Miradi ya Uimarishaji wa Usafiri wa Baharini ambapo kwa kipindi kilichopita kutokana na sababu mbali mbali miradi hii haikukamilishwa na baadhi yake haikuanza kutekelezwa kabisa. Miongoni mwa miradi ambayo Kamati inasisitiza ni pamoja na Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Karume Pemba, Ujenzi wa Barabara ya Wete – Chake Ckake na Barabara ya Chake Chake – Mkoani ili huduma za usafiri katika kisiwa cha Pemba ziweze kuimarika na kupelekea azma ya Serikali ya kuifanya Pemba kuwa eneo maalum la uwekezaji liweze kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha Sekta ya Utalii, pamoja na maeneo yaliyoainishwa kutekelezwa, Kamati inasisitiza umuhimu wa kushirikishwa ipasavyo kwa sekta binafsi katika kukuza utalii nchini na kujenga uchumi wetu kwa kuhakikisha changamoto wanazokabiliana nazo zinatatuliwa pamoja na kuiwekea mazingira bora sekta ya hii.

## MWELEKEO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Mheshimiwa Spika, Mwelekeo wa Mapato na Matumizi kwa mwaka 2022/2023 yanakadiriwa kufikia jumla ya TZS 2,207. 2 bilioni ambayo yanatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani, misaada na mikopo kutoka kwa washirika wa maendeleo na Mikopo ya ndani na ya nje kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, kwa upande wa Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka vyanzo vyake vya ndani yanatarajiwa kukusanywa ni jumla ya TZS 16.7 bilioni.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia kwamba mwenendo wetu wa ukusanyaji mapato haujawa wa ufanisi, na hapa Serikali inaweka matarajio ya juu ukilinganisha na mwaka uliopita, Kamati inaitaka Serikali kuweka bayana hatua na mikakati iliyoweka ili kufikia lengo hilo. Ni vyema tukajua kwamba matarajio haya yana uhalisia au ni makisio ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato Kamati inaishauri Serikali kuweka mkazo zaidi katika Kuendelea kuimarisha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji, Kupanua wigo wa kodi na kujenga mahusiano na mazingira rafiki kwa mlipakodi, Kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi, Kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji mapato kwa Wizara na taasisi za umma, Kuhimiza matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato yakijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha kwa upande wa matumizi, Serikali ihakikishe inaendeleza mikakati ya kudhibiti nidhamu ya matumizi ya fedha za umma na kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele yatakayochochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu.

MAONI NA USHAURI WA JUMLA

Mheshimiwa Spika, Kwa azma ya kuijiongezea mapato na kuwainua wananchi wa Zanzibar kiuchumi, Kamati ya Bajeti inaishauri Serikali ianze kuweka mikakati katika Sekta ya Fedha za Kiislam (Islamic Finance) kwani tafiti zinaonesha kwamba nchi nyingi zimenufaika kwa kiasi kikubwa katika kutumia mfumo huo. Mfano wa wanufaika wakubwa ni nchi ya Nigeria ambayo inapata fedha za kuimarisha miundombinu na hatimae kupunguza kuendelea kukopa fedha za miradi.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Rasilimali watu ni jambo muhimu ili nchi iweze kupiga hatua za kimaendeleo. Ili malengo na mafanikio ya nchi yafikiwe, ni lazima kuwepo na uwezeshaji wa watendaji katika kuwajengea uwezo wa kitaaluma na ujuzi sambamba na kuimarisha maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, Ukuaji endelevu wa uchumi unatakiwa uweze kutengeneza fursa za ajira, ambazo zitapelekea kupunguza umaskini na utegemezi kwa kuufanya ukuaji huo wa uchumi uwe shirikishi zaidi. Kutokuongezeka kwa fursa za ajira hususan kwa vijana kunapunguza kasi ya kupungua kwa umaskini. Vijana ndio injini ya maendeleo ya nchi yoyote ile duniani kwani ndio nguvu kazi ya kutegemea na hawapaswi kuwa

tegemezi na kuwachwa mkono.

Mheshimiwa Spika, Jambo la mwisho katika mambo ambayo Kamati inashauri ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato ni kutafuta utatuzi wa haraka wa mkwamo wa usafirishaji wa bidhaa kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Kuwajengea mazingira wezeshi wafanyabiashara wetu ili walipe kodi kwa hiyari.

## HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Kwa kumalizia napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako kwa kunipa nafasi kwa kuwasilisha Hotuba ya Mapendekezo ya Mapango wa Maendeleo na Mwelekeo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa utulivu wao na kwa usikivu wao katika kipindi chote nilichokuwa nawasilisha maoni ya Kamati. Aidha, naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa ushirikiano na ustahamilivu wao wakati tukitekeleza majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Ili kuzipa uzito shukurani zangu kwa Wajumbe wa Kamati, naomba uniruhusu niwataje kwa majina yao kama ifuatavyo:

1. Mhe. Ali Suleiman Ameir (Mrembo) Mwenyekiti
2. Mhe. Anna Athanas Paul Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Harusi Said Suleiman Mjumbe
4. Mhe. Issa Haji Ussi Gavu Mjumbe
5. Mhe. Miraji Khamis Mussa Mjumbe
6. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Mjumbe
7. Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad Mjumbe

Mheshimiwa Spika, Aidha napenda kuishukuru Sekreteriati ya Kamati ya Bajeti kwa ushirikiano mzuri, ushauri na miongozo wanayoipatia Kamati yangu. Naomba nao niwashukuru kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:

1. Ndg. Asha Said Mohamed Katibu
2. Ndg. Shaib Fadhil Shaib Katibu

3. Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi — Katibu

4. Ndg. Yustina Edward Joseph — Msaidizi wa Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waichangie Hotuba hii pamoja na kuishauri Serikali katika utekelezaji mzuri wa Mpango huu.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

Ahsante,

…………………………………

Mhe. Ali Suleiman Ameir,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar.